



Mipango ya Msaada wa Wateja Ni gani inayokufaa?

Jiunge na maelfu ya wateja wanaopata msaada wa bili zao za kila mwezi! Mipango yetu ya Msaada wa Wateja inatoa msaada wa fedha kwa wateja wakazi wenye mapato yanayostahiki wanaotatizika kulipa bili yao ya PGH2O. Chaguo nyingi zinapatikana, na hakuna yeyote anayepaswa kuchagua kati ya kulipa bili yake ya maji/maji taka na gharama nyingine muhimu. Ili kujadili chaguo zinazokufaa, tafadhali wasiliana na timu yetu ya PGH2O Cares kwa nambari **412-255-2457** au tuma barua pepe kwa timu hiyo katika cares@pgh2o.com.

Mpango wa Punguzo la Bili (BDP, Bill Discount Program): Kwa wateja wanaopata mapato yanayolingana na au yaliyo chini ya asilimia 150 ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali ya Shirikisho (FPL, Federal Poverty Level), hulipishwi gharama ya galoni zako 1,000 za kwanza za maji na huduma ya usafirishaji wa maji taka, na unalipa asilimia 15 pekee ya ada ya kila mwezi ya maji ya mafuriko. Kwa wateja wanaopata mapato yanayolingana na au yaliyo chini ya asilimia 50 ya FPL, unapata pia punguzo la asilimia 50 ya gharama yako ya matumizi ya zaidi ya galoni 1,000 za maji. Ikiwa unastahiki, una deni na uko kwenye mpango wa malipo unaofanya kazi, unapata punguzo la \$30 kila mwezi kwa kila malipo unayolipa kwa wakati unaofaa ili kupunguza deni la zamani unalodaiwa.

Ruzuku za Shida ya Fedha + Fedha za Msaada wa Maji Safi (CWAFF, Clean Water Assistance Fund): Wateja wanaopata mapato yanayolingana na au yaliyo chini ya asilimia 150 ya FPL wanaweza kustahiki kupata ruzuku ya hadi \$300. Timu yetu ya Cares inaweza pia kukusaidia kutuma ombi la ruzuku ya ALCOSAN ya Fedha za Msaada wa Maji Safi.

Mipango ya Malipo na Msamaha wa Deni: Mipango ya malipo inayotokana na mapato inapatikana ili kuwasaidia wateja wakazi na wamiliki wa biashara ndogo kulipa madeni makubwa bila kutozwa ada za kuchelewa kulipa. Wateja wakazi walio kwenye Mpango wa Punguzo la Bili (Bill Discount Program) na wana deni la zamani wanalodaiwa watapata punguzo la \$30 kwa kila malipo wanayolipa kwa wakati unaofaa wakiwa wamejiandikisha kwenye mpango wa malipo unaofanya kazi.

Ruhusa ya Kukawia Kulipa Deni katika Majira ya Baridi (WM, Winter Moratorium): Wateja wanaopata mapato yanayolingana na au yaliyo chini ya asilimia 300 ya FPL wanaweza kustahiki kulindwa kutokana na kukatiwa huduma ya maji katika miezi ya majira ya baridi ya Desemba hadi Machi.

Mpango wa Fidia ya Ubadilishaji wa Bomba la Maji Lililotengenezwa kwa Madini ya Risasi (LSLRP, Lead Service Line Replacement Reimbursement Program): Unapoamua kutafuta mwenyewe fundi wa mabomba ili abadilishe bomba la maji lililotengenezwa kwa madini ya risasi, unaweza kustahiki kupata fidia ya baadhi ya gharama hiyo. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea lead.pgh2o.com/leadreimbursement.

Mwongozo wa Mapato wa Kila Mwaka wa 2023

Idadi Watu Wanaoishi Nyumbani	50% ya FPL	150% ya FPL	300% ya FPL
1	\$7,290	\$21,870	\$43,740
2	\$9,860	\$29,580	\$59,160
3	\$12,430	\$37,290	\$74,580
4	\$15,000	\$45,000	\$90,000
5	\$17,570	\$52,710	\$105,420
6	\$20,140	\$60,420	\$120,840
7	\$22,710	\$68,130	\$136,260
8	\$25,280	\$75,840	\$151,680
Kwa kila mwanafamilia wa ziada ongeza:	\$2,570	\$7,710	\$15,420

Ili upate maelezo zaidi kuhusu mipango hii na huduma nyingine za msaada, tafadhali tembelea www.pgh2o.com/CAP.



Penn Liberty Plaza 1
1200 Penn Avenue
Pittsburgh, PA 15222
www.pgh2o.com

Huduma kwa Wateja*
Simu 412.255.2423 (Teua Chaguo la #5)
Faksi 412.255.2475
info@pgh2o.com

Huduma ya Dharura*
Simu 412.255.2423 (Teua Chaguo la #1)
Inapatikana wakati wowote,
mchana au usiku

• Translation services available |
• Servicios de traducción disponibles |
• 提供翻译服务 | • Доступны услуги перевода |
• خدمات الترجمة متوفرة